MUJADDID WA ZAMA ZETU, IMÂM AL-ALBÂNI

[*rahimahullâh*]

NA KUMSIFU KWAKE MWANAFUNZI WAKE MUHESHIMIWA, SHEIKH 'ALI HASAN AL-HALABÎ AL-ATHARÎ, NA SHAHADA ZA IMÂM AL-ALBÂNI JUU YA UMAHIRI WAKE KATIKA TA'LUMA YA MANHAJ NA HADÎTH

---

1. Mujaddid wa zama zetu hizi, Imâm al-Albâni alisema katika mwaka wa 1412 AH (1991 CE), ulipokuwa ni wakati baadhi yetu bado tulikuwa kwenye shule za msingi: **"Nilipeana copy hiyo kwa rafiki yetu na aliye mwanafunzi, kijana 'Ali bin Hasan al-Halabî,** ili iwe tayari kusambazwa ikiwa na utangulizi wa kiusomi ulioandikwa kwa faida ya wasomaji watukufu. Na yeye ndiye aliyefanya yote haya, **twamuombea Allâh Amzidishie kheri**, na kisha yeye ndiye aliyesimamia uchapishaji wake, uswahihishaji na pamoja na kuipitia[2].

2. **"Rafiki yake kalamu iliyo na Rehma nyingi, mwalimu 'Ali bin Hasan al-Halabî, Abi'l-Hârith."**[3]

---

[1] http://www.alalbany.name/audio/664/664_33.rm - Hapa Imâm al-Albânî alikuwa akimtetea Sheikh 'Ali bin Hasan al-Halabi al-Atharî, akimwambia muulizaji-butu aliyekuwa akiulizia kuhusu baadhi ya mambo kutoka katika *Anwâr ul-Kâshifah:*

> **"Wewe ulimuanza 'Ali na ukamalizia na al-Albânî!? Huu ni ushahidi yakwamba wewe hupitii kwenye njia swahîh ya 'ilmu! Ulimuanza 'Ali!? Sasa wataka nini ulipomuanza 'Ali?Sasa mimi nakuuliza wewe: wataka nini kwa 'Ali? Suali lako ni lipi? Allâh na Akuongoze! Wewe wazungumza kumuhusu 'Ali, na wala sio al-Albânî? Kazi yako ni kufuatilia makosa tu! Yakuhusu nini wewe ikiwa mwanafunzi wangu ametatizika?!"**

Kisha Imâm al-Albânî akamaliza majadiliano hayo akimwambia muulizaji yakwamba yeye hapotezi wakati wake na watu wasiokuwa na 'ilmu wakawa hawayajali mas'ala yenye umuhimu!

[2] *Hukmu Târik us-Swalât* Uk.25

[3] *As-Silsilat us-Swahîhah,* Muqaddimah Vol.6

3. Mujaddid wa zama zetu hizi, Imâm al-Albâni (*rahimahullâh*) amesema katika *as-Swahîhah* (*vol. 2, Uk.720*) katika kusifu ukosoaji wa urongo wa muharibifu wa Sunnah, Hassân 'Abdul-Mannân: "... katika kuwasilisha mazungumzo yenye kubainisha mtiririko wa maneno yake yote yanayohusiana na udhaifu wake kunahitaji kuandikwe kitabu maalum, na muda wangu hauniruhusu mimi kwa sasa. **Kwahivyo huwenda labda baadhi ya ndugu zetu walio na nguvu katika 'ilmu hii wanaweza kutekeleza hayo, kama vile ndugu 'Ali al-Halabî ...".** Vilevile tizama utangulizi wa *at-Ta'lîqât ar-Radiyyah 'alar-Rawdah an-Nadiyyah*, chapa ya al-Maktabah al-Islâmâyyah ya *Aadâb az-Zifâf, na an-Naswihah*.

4. Amesema Imâm al-Albâni katika utangulizi wa kitabu chake *at-Ta'lîqât ar-Radiyyah 'alar-Rawdah an-Nadiyyah:* **"Zaidi ya miaka miwili iliyopita mtoto wetu na rafiki yetu, ndugu Abu'l-Hârith 'Ali bin Hasan bin 'Ali al-Halabî, Allâh Amuafikiye, alinishauri kwa fikra ya kukipiga chapa hicho kitabu kilichotajwa cha Ta'lîqât na kukisambaza.** Alitoa shauri hilo kutokana na faida alizoziona ndani yake, na kwahivyo itabakia kama mtego tu kwenye rafu la vitabu ili wanafunzi na wale wenye ufahamu mzuri waweze kufaidika nacho. Kwahivyo mimi nikakubaliana na shauri hilo na nikampa nakala yangu binafsi yenye sherehe yangu ndani yake kwa khati zangu na nikakiita *at-Ta'lîqât ar-Radiyyah 'alar-Rawdah an-Nadiyyah*, **ili apate kuanzia na shughuli hii ya umuhimu – namuombea Allâh amzidishie kheri nyingi.** Na kitabu ndicho hiki hapa kikiwa na sherehe yake, na katika kumsifu Allâh na baraka Zake, imechapishwa kwa mkono wa wasomaji, ili wapate kufaidika kutokana nacho na wapate faida zake. Kila sifa njema zinamstahiki Allâh, Mwenye kukamilisha matendo mema, **Namuomba Allâh (تبارك وتعالى) amlipe rafiki yetu, Abu'l-Hârith, Allâh Amuafikiye katika kufuzu, kwa juhudi zinazostahiki sifa katika kuifanyia tahkiki sherhe kwa kuidhihirisha kuwepo kwake."**

5. Alisema Imâm al-Albâni (*rahimahullâh*) alipokuwa akimnaswihi Abu Ruhayyim: **"Lau kama 'aqîdah yako ni kama 'aqîdah ya Mashekhe watatu ambao wewe (unaodai) kuwatetea, ambao ni Ibn Bâz, Ibn 'Uthaymîn na al-Albâni, basi 'aqîdah ya ndugu 'Ali ni sawa na aqîdah yao! Lakini ikiwa aqîdah yako itakhalifiana na hiyo aqîdah ya ndugu 'Ali, basi mimi niko tayari kukaa na wewe (ili tuibadilishe aqîdah yako)! ..."**[4]

6. Amesema ndugu 'Azmî al-Jawâbirah, katika kitabu chake *Mâdhâ Yanqumûna min al-Îmâm al-Albâni?* (Uk.14) yakwamba: "Nilimuuliza mwalimu wetu, Sheikh Nâsir, kuhusu upinzani wa Abu Ruhayyim dhidi ya Sheikh 'Ali. Akajibu Sheikh wetu (*rahimahullâh*) kwa matamshi machache tu, na Allâh ni shahidi kwa ninayoyasema, yakwamba: **"Ndugu 'Ali ni sawa na watu elfu-moja-na-moja mfano wa Abu Ruhayyim!"**

[4] Yametajwa na ndugu Muheshimiwa na mwalimu Abû 'Abdullâh 'Azmî al-Jawâbirah, Allâh Amuhifadhi, tarehe: 20 Rabî' ul-Awwal 1422 AH/ Jumatatu 11 June, 2001 CE na kushuhudiwa na ndugu Lâfî Shatrât na Kâmil al-Qash-Shâsh.

7. Sheikh, Dr. Ahmad bin Sâlih az-Zahrânî (Abû ‘Umar al-Kinânî) alisema katika matangazo chini ya anwani *‘Abul Hârith, kuanzia mwanzoni nilijihisi kumuonea wivu!!’* katika ukumbi wa mtandao wa sahab, tarehe 2nd May, 2001 CE, kuhusiana na mwenye kuonyesha uadui kwa Sheikh ‘Ali Hasan, katika wakati huo, Abu Ruhayyim: **“Naam, ni wivu na wala sio furaha. Kwahivyo tunauliza, ni kwanini basi iwe hivyo? Ni kwa sababu ya mapenzi makubwa sana niliyoyaona na kuyasikiya kutoka kwa Sheikh Nâsirud Dîn al-Albânî (*rahimahullâh*) akikukusudia wewe na utegemezi wake juu yako na mkuruba wake kwako wewe. Allâhu Akbar! *Wallâhi,* Sheikh hazungumzi kuhusu suala lolote wala hutoweza kusikiya mkusanyiko wowote isipokuwa utakuwa ukisikiya mara kwa mara: “Yuko wapi Abu’l-Hârith?”; “Hebu tumsikiye naye Abu’l-Hârith; “Ndio Ewe Abu’l-Hârith”; “Una lipi (la kusema) Ewe Abu’l-Hârith?”; “Yaonekana kana kwamba Abu’l-Hârith ataka kuongezea kitu”; “Au sivyo, Ewe Abu’l-Hârith?” Kwahivyo nikasema: Pongezi kwako, Ewe Abu’l-Hârith, na ni kubarikiwa kulioje kwa kuwa na mkuruba sampuli hii na ‘ilmu hii, Ewe Abu’l-Hârith! Lau kama ningelikuwa na nafasi kama hii yako, hilo lingelikuwa ni bora kwangu kuliko kuchukuliwa maisha yangu yote ya kilimwengu! Kila ninaposikiya mikusanyiko kama hii (kwenye kanda za tepu), mimi moja kwa moja hukumbuka kuhusu madai yakwamba ati al-Halabi si miongoni mwa wanafunzi wa al-Albâni, na ati yeye ni kadhaa na kadhaa na kwamba yeye ni hivi na hivi!! Kwahivyo mimi hujichekea na husema: Kuna dalili gani iliyo zaidi ya hii? Bali husema: Huu ni ushahidi kamili wa mafungamano makubwa ya Sheikh al-Albâni, mkuruba na uaminifu kwa Abu’l-Hârith.** Kwa hakika, niliyoyapata kutokana na kanda hizi ni kwamba Abu’l-Hârith amepewa ‘ilmu na na akabarikiwa kwenye ‘ilmu hiyo, kwani yeye alikuwa ni mmahiri katika kujibu kwenye vikao vya Sheikh kuhusu taarifa ambazo hapana awezae kuongezea isipokuwa mtu hodari sana. Kwa ujumla, usifikirie yakwamba mimi nina wivu na wewe! Mimi najaribu kuifahamisha hali ya baadhi, wala sio wote wenye kukushambulia na kukutuhmu wewe. Kwahivyo, nawaamkuwa nyote ndugu zangu katika Markaz al-Albâni!”

8. “Rafiki yetu Muheshimiwa ‘Ali al-Halabi ametaja katika kitabu chake chenye faida nyingi *Tanwîr ul-‘Ayn’ayn* (Uk.17-27) kauli Kumi na Nne kutokana nazo na itadhihirika kwa kila atakayeziona yakwamba baadhi yao huwafuata wengine ki-Upofu na kwamba hujiingiza kwenye mas’ala ambayo hawana ujuzi uanaohusiana nayo.”[5]

9. **“Kwahiyo, aliyehusishwa hapo, amemshutumu rafiki yetu ‘Ali al-Halabi kwa sababu alikuwa akitafuta kuthibitisha nguvu ya hadîth ya ‘Âishah kwa maneno ya al-Hâfidh katika *at-Talkhîs* ...”** kisha Imâm al-Albâni, mujaddid wa zama zetu hizi, akasema kumuhusu mwenye kumkashifu Sheikh ‘Ali al-Halabi al-Atharî: **“Hizi ni shutuma zilizo bâtwil zilizoegemezwa juu ya ujinga mtupu katika ta’luma hii tukufu na Usûli wake.”[6]**

[5] *Radd ul-Mufhim,* Uk.79, Nukta ya Chini No.1
[6] Ibid., Uk.89

10. “Kwani Suleimân bin Bilâl ni mtu aliye ‘Thiqah’ na ni ‘Hujjah’, matumizi ya hadîth hii ni ambayo iliyoafikiwa kulingana na Sheikhayn na wengineo na wala hakukosolewa kwa tadlîs. Sasa itakuwaje sawa kuidho’ofisha hadîth yake kama alivyofanywa na ‘Abdullâh, wakati ambapo yeye (‘Abdullâh) ni dha’ifu?! **Na ndugu ‘Ali al-Halabi amemkosoa vizuri sana pamoja na ambayo aliyoyaambatisha, twamuombea Allâh amjazi kheri.”**[7]

11. Mujaddid wa zama zetu hizi, Imâm al-Albâni (*rahimahullâh*) amesema amesema kuhusu baadhi ya *ahâdîth*: “Pana uwezekano yakwamba zinapatikana kwenye baadhi ya nakala za al-Musnad, na imenifikia mimi kutoka kwa baadhi ya ndugu zetu wenye kushughulika kwenye ta’luma hii tukufu yakwamba alipata kipande chake ambacho kilikuwa hakijachapishwa, kwahivyo pana uweekano yakwamba hadîth inapatikana ndani yake. Sasa ikiwa inapatikana ndani yake, basi inawezekana zaidi kupitia kwa njia ya mkondo wa hii ‘Atrâf. **Fahamu zangu zimeliwaza jambo hili kama ambavyo ndugu ‘Ali al-Halabi alivyonifaidisha mimi katika suala hili kwa njia ya simu, Allâh amjazi kheri,** aliponipasha yakwamba al-Hâfidh Ibn Hajar aliipata hadîth hiyo katika Atrâf ul-Musnad (vol.1; Uk.48; No.84 – *tahqîq* ya ndugu Samîr).”[8]

12. Mujaddid wa zama zetu hizi, Imâm al-Albâni (*rahimahullâh*) alisema alipokuwa akiwasilisha maneno yake juu ya Sheikh Ismâ’îl al-Answârî, Allâh Amswamehe: **“Niya yangu ndani ya utangulizi huu sio kumkosoa juu ya haya madai mawili ya urongo <u>kwa sababu ndugu muheshimiwa ‘Ali Hasan bin ‘Abdul-Hamîd amenitosheleza mimi kutokamana na hayo katika risala yake ya nguvu kwa kuinukuu risala iliyotajwa hapo juu ya al-Answârî ambapo ndani yake ameyataja makosa mengi.</u> Kwahivyo yoyote atakae kuujuwa ukweli na akiregelee kwani kwa hakika mtu atajionea mwenyewe tafauti ya wazi baina ya ukosoaji wa al-Answârî na mashambulizi juu yangu na baina ya ukosoaji wa rafiki yetu juu yake na adabu aliyomuhishimu nayo ambayo al-Answârî hakustahiki kupewa kutokana na uadui wake wa kuendelea na dhulma.”**[9]

13. Amesema Imâm al-Albâni alipokuwa akizungumzia kuhusu baadhi ya ahâdîth: “Haya ndiyo niliyoandika zaidi ya takriban miaka Kumi iliyopita, kabla ya kitabu *ath-Thiqât* cha Ibn Hibbân hakijachapishwa. **Kisha nikaja kugundua uswahihishaji wa hadith ulioandikwa kwa mkono wa ndugu ‘Ali al-Halabi aliyerekebisha makosa ya uchapishaji na akaandika nukta kwenye sehemu ya upande wa hiyo hadith, Allâh amlipe kila la kheri ...”**[10]

14. “Nimeziswahihisha baadhi ya ahâdith hizo ambazo ni mifano inayolingana ambayo as-Sakhâwî (*rahimahullâh*) aliyoitaja, tizama hadith ifuatayo No. 6919 na

[7] As-Silsilat us-SwahÎhah; Vol.6, Uk.137
[8] As-Silsilat us-SwahÎhah; Vol.6, Uk.401
[9] As-Silsilat udh-Dhwa’ifah, Vol.8, Uk.1
[10] Ibid., Vol.3; Uk.628

yanayofuata baada yake. **Kwa ajili hii, ndugu yetu Abu'l-Hârith al-Atharî ametekeleza kazi nzuri katika kuziepuka ahâdîth zilizo *dha'îf* kutoka katika *Mukhtasar* wake, kwa jina la** *al-Muntaqâ an-Nafîs min Talbîs Iblîs.*"[11]

15. Imâm al-Albâni (*rahimahullâh*) amesema katika kuzungumzia kuhusu baadhi ya ahâdîth alizozitumia katika kumkosoa Sheikh Hamûd at-Tuwayjurî (*rahimahullâh*) kuhusu yaliyo kwenye kitabu chake *as-Sârim al-Mash-hûr*: **"Baada ya kuandika yaliyopita, nilifaidika kutoka kwa ndugu 'Ali al-Halabi, Allâh amjazi kila la kheri,** yakwamba hadith imepokewa na al-Bahhâr katika Musnad yake. Kwahivyo, nikairegelea kwake na kuiona yakwamba ina nguvu kwa upande wa al-Hamânî.[12]

16. Imâm al-Albâni (*rahimahullâh*) amesema: "Hadith hii imenukuliwa na as-Suyûti na nyongeza yake katika, *ad-Durr al-Manthûr*, kutoka katika riwaya ya Ibn al-Mirwadayh, **na ndugu yetu 'Ali Hasan al-Halabi akainasibisha naye, kwa kunukuu kutoka kwa ad-Durr, kisha yeye (Sheikh 'Ali Hasan) akaitaja hii katika** *at-Ta'qîb 'alâ Risâlat a-Answârî* **alipokuwa akizungumzia kuhusu hadith iliyo mashuhuri sana ya 'Atiyyah: "Yâ Allâh, nakuomba kwa haki za wenye kukuomba!" (Uk.25). Alisema katika kuyafafanua haya, "Mimi nasema: inaonekana kana kwamba hii vilevile inatokamana na riwaya ya al-'Awfiyy, lakini hiyo ni dhana tu, kwani mimi sijaiona silsila yake haswa ya upokezi. "Kwahivyo yeye alipatia, kama muonavyo, Allâh amjazi kila la kheri!"**

Katika kitabu chake, *Safahât Baidhâ' min Hayât al-Imâm Muhammad Nâsiruddîn al-Albânî* (San'â' Yemen: al-Maktabah al-Islâmiyyah, 2001), Uk.56, Sheikh 'Atiyyah Sâlim ametaja:

> **'Ali Hasan 'AbdulHamîd al-Halabi: ndiye maarufu zaidi miongoni mwa wanafunzi wa Sheikh leo hii, na ni miongoni mwa wenye nguvu zaidi katika wanafunzi wa ki'ilmu** – Na mimi namzingatia yeye kuwa hivyo, na wala simdhamini yeye zaidi ya Allâh. Yeye ni msomi wa kikweli na muaminifu, anazo *rasâ'il* nzuri na vitabu. Mimi nimewahi kuonana naye, tukakaa pamoja mara nyingi na nikamuona kuwa ni mchangamfu, mpole na daima ni mwenye furaha.

Vilevile ametaja (katika Uk.52):

> Katika Mji wa Abu Dhabi, Lu'ay bin 'Abdir-Razzâq Nâsir ud-Din al-Albânî alinihadithia kwa kusema, "Nilimsikiya 'Ubâdah, mjukuu wa Sheikh al-Albânî akimuuliza babu yake wakati wa miezi yake ya mwisho kuhusu watu wema wawili katika ta'luma ya hadith, leo hii. Sheikh akamjibu, 'Ali Hasan al-Halabi na Abû Is-hâq al-Huwaynî."

Mfasiri: Abu Farida Muhammad Awadh Salim Basawad
http://www.qssea.net
Mombasa. Kenya

[11] Ibid., Vol.3; Uk.181
[12] Ibid., Vol.3; Uk.540